



MASENO UNIVERSITY
UNIVERSITY EXAMINATIONS 2016/2017

**SECOND YEAR SECOND SEMESTER EXAMINATION FOR
THE DEGREE OF BACHELOR OF ARTS IN KISWAHILI
WITH INFORMATION TECHNOLOGY**

CITY CAMPUS – SCHOOL BASED

AKI 204: KISWAHILI POETRY

Date: 19th December, 2016

Time: 3. 00 - 6.00pm

MAAGIZO:

- Jibu Maswali Matatu: Swali la Kwanza ni la Lazima.

1. A) Eleza mihimili muhimu ya nadharia ya umuundo
b) Chambua shairi lifuatalo Kimuundo

(AL 26)

PENDO LA PESA

Pendo la pesa si pendo, mbali nalo jitengee
Pendo lanuka uvundo, mbali nalo lisogee
Pendo halina uhondo, katu usilicheke
Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo

Pendo halina utamu, lina harufu jemee
Pendo ninalilaumu, mimi lisinilemee
Pendo halina kudumu, hadi pesa umwekee
Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo

Pendo lataka kupenda, bila kupiga kengee
Pendo mfano wa tunda, ukila unenepee
Pendo la pesa huvyonda, tupa usilipokee
Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo

Pendo la kwa kila hali, ubora na lipotee
Pendo kutumia mali, ndipo aitike bee
Pendo hilo ni dhalili, mbali nalitokomee
Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo

Pendo kutumia hela, mifuko iteketee
Pendo hilo lahaula, ni zigo ujibebee
Pendo wawili ni kula, nyama ndimi mnenee
Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo

Pendo kwa watu chaguo, lazima nielezee
Pendo ni sawa funguo, kufuli imngojee
Pendo la kupenda nguo, bora lichekwe heehee
Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo

Pendo ni la pale zama, wanahadithi wazee
Pendo lao likiuma, bila kusema nige
Pendo sasa limelema, ukipanda lisimee
Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo

Pendo hapa nakomesha, mbele nisiendele
Pendo la pesa nafisha, ni gonjwa usipokee
Pendo hadhi linafisha, la pesa sipendele
Pendo halina sheree, pendo la pesa si pendo

2. Fafanua kikamilifu mgogoro wa ushairi wa Kiswahili na hoja zilizotolewa na kila upande kujitetea (AL 22)
3. Asili ya ushairi wa kiswahili ni ushairi simulizi wa kibantu” Thibitisha (AL 22)
4. Eleza sababu zinazofanya ushairi kuendelea kuwepo katika jamii (AL 22)
5. Maudhui ya ushairi wa Kiswahili yamekuwa yakibadilika kama ambavyo wakati ulibadilika” Thibitisha. (AL 22)
6. Taswira ni mbinu muhimu inayomsaidia mwandishi wa Al-Inkishafi kuwasilisha ujumbe wake. Jadili (AL 22)